*Kioo cha Lugha, Juz. 20(1), 130-149*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i1.9

# Mchango wa Mathias Mnyampala katika Maendeleo ya Ushairi wa Kiswahili

*Anna N. Kyamba*[1]

**Ikisiri**

Makala hii inakusudia kuchunguza mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mnyampala ni miongoni mwa washairi maarufu wa ushairi wa Kiswahili katika karne ya ishirini. Kwa ujumla, mchango wa Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili haujulikani kikamilifu tukilinganisha na washairi wengine kama Muyaka bin Haji na Shaaban Robert. Maswali tunayojiuliza ni kwamba: kwa nini Mnyampala hajazungumziwa na wataalamu mbalimbali? Mnyampala alikuwa na mchango gani katika ushairi wa Kiswahili? Kutokana na maswali hayo tunaona kuna haja ya kuchunguza mchango wa mtaalamu huyu katika ushairi wa Kiswahili. Hivyo, katika makala hii tunabainisha mchango wa Mnyampala (akiwa mshairi wa mwanzo wa miaka ya 1960 anayetoka sehemu za bara) katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kimaudhui na kifani. Data zilizomo ndani ya makala hii zimetokana na mbinu ya maktabani na mahojiano na watafitiwa nyanjani kuhusu maisha, historia ya Mnyampala, kazi zake zilizochapishwa na miswada yake isiyochapishwa ambayo ni: *Hazina ya Washairi*, *Mahadhi ya Kiswahili* na *Mashairi ya Vidato*.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii imeshughulikia mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Watafiti mbalimbali wamechunguza kazi za Mnyampala kwa namna mbalimbali. Baadhi ya watafiti hao ni Madumulla (2011), Makaka (2012), Mgute (2012), na Roy (2014). Kutokana na ufinyu wa sampuli, mahitimisho yanayotolewa na watafiti hao yanazua maswali kuhusiana na mchango wa mtunzi huyu katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Aidha, watafiti wengi waliotangulia wamejikita katika kuchunguza kazi za ushairi zilizochapishwa za Mnyampala na kuziacha kazi zisizochapishwa. Mathalani, Mgute (2012) amechunguza mchango wa Mathias Mnyampala katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Mtafiti huyu ameangazia kazi tano teule za Mnyampala ambazo ni: *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Waadhi wa Ushairi* (1965), *Ngonjera za UKUTA 1* (1970), *Ngonjera za UKUTA 2* (1971) na *Kisa cha Mrina Asali na Wenzake Wawili* (1982). Mgute aliangalia mchango wa Mnyampala katika fasihi

[1] Mhadhiri, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: annanicholausk@gmail.com

kiujumla mno na kujiegemeza katika kazi za mashairi zilizochapishwa tu. Mtafiti huyu ametaja baadhi ya vipengele vya fani na maudhui pasi na kufanya uchambuzi wa vipengele hivyo. Haya yanajidhihirisha katika mapendekezo yake anapoeleza kuwa kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu vipengele vya fani na maudhui pamoja na tungo ambazo hazijachapishwa ili kubaini mchango wa Mnyampala kikamilifu. Mapendekezo hayo, yalitupatia msukumo wa kuandika makala hii ili kubaini mchango wa mshairi huyu katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Katika kutathmini mchango huo, kwa kiasi kikubwa, tumeangazia vipengele mahususi vya fani na maudhui vilivyojitokeza katika kazi zake.

## 2.0 Fani

Dhana ya fani imefafanuliwa na wahakiki mbalimbali. Baadhi yao ni Madumulla (2009), Senkoro (2011) na Mulokozi (2017). Wataalamu hawa wanasema kuwa fani ni ufundi wa kisanaa anaoutumia msanii kuwasilisha kazi yake kwa hadhira. Wataalamu hawa wanadai kuwa fani hujumuisha wahusika, mandhari, lugha, mtindo na muundo. Katika makala hii vipengele vya fani vilivyochunguzwa ni mtindo na muundo.

### 2.1 Mtindo

Katika ushairi wa Kiswahili, mtindo umefafanuliwa na watafiti mbalimbali. Baadhi yao ni Mulokozi (2017) na Njogu na Chimerah (1999), ambao wanadai kuwa mtindo wa mshairi hujidhihirisha katika matumizi yake ya lugha, kama vile uteuzi na upangaji wa maneno, mpangilio wa sauti za lugha ili kuleta athari fulani, matumizi ya tamathali za semi kama vile tashbiha, sitiari, mafumbo tasfida na nyinginezo. Naye Wamitila (2004) anaeleza kuwa mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji ama wasikilizaji wa kazi husika. Kadhalika, Samwel na wenzake (2013) wanabainisha kuwa mtindo ni upangaji wa fani na maudhui kwa namna ambayo inampambanua mshairi mmoja na mwingine. Wanaongezea kuwa mtindo huchunguza endapo shairi ni la tathlitha, tarbia, takhmisa, sudusia na mitindo mingineyo. Kutokana na mawazo ya wataalamu mbalimbali tunaweza kusema kuwa mtindo ni ufundi anaotumia mwandishi katika kuiumba kazi yake ili iweze kueleweka na walengwa wa kazi hiyo. Hivyo basi, mtindo hujumuisha mbinu za kiuandishi, matumizi ya lugha, tamathali za semi na mbinu nyingine za uandishi. Kwa ujumla, Mnyampala kama mmoja wa waandishi wa kazi za fasihi, hususani katika ushairi wa Kiswahili, hakuwa nyuma katika kukikabili na kukimudu kipengele hiki cha mtindo katika kazi zake za ushairi. Katika kipengele hiki cha mtindo, mchango wake katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili umejitokeza kama ifuatavyo:

#### 2.1.1 Mtiririko

Mnyampala alibuni mitindo mbalimbali ya utunzi wa ushairi wa Kiswahili. Ndiye aliasisi mtindo wa mtiririko. Mtindo huu hubainisha mashairi ambayo vina vyote vya kati vya mistari mitatu ya kila ubeti hufanana kutoka mwanzo hadi mwisho, na

vile vya mwisho vya mistari mitatu ya mwanzo navyo hufanana kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho na katika kibwagizo hubadilishana vina[2]. Madumulla (2011) anaeleza kuwa Mnyampala ndiye aliyeanzisha mtindo wa mtiririko na msisitizo. Naye Charles Mnyampala (2014) anaeleza kuwa mtindo wa mtiririko humtaka mshairi ambaye ni tajiri wa msamiati wa Kiswahili asitindikiwe na urari wa vina. Katika *Diwani ya Mnyampala* alitunga shairi lenye kichwa "Tungeni Mtiririko" (uk. 5), anasema:

Mhariri mahabubu, pokea wangu mwandiko,
Napenda kuwa hotubu, washairi walioko,
Si kama nawaghilibu, na kujitia vituko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Katika shairi hili mwandishi alikuwa anahimiza watunzi wenzake watunge kwa kutumia mtindo wa mtiririko. Katika ushairi huu toka ubeti wa kwanza hadi mwisho, vina vya katikati ni "bu" na vina vya mwisho ni "ko" lakini katika kibwagizo kina cha mwisho kimekuja kati na cha kati kimeenda mwisho. Hivyo, katika kibwagizo, kina cha kati ni "ko" na mwisho ni "bu." Kwa kawaida, utunzi wa namna hii unahitaji mtu ambaye ni mbobevu katika lugha, vinginevyo kutakuwa na utungaji wa kikasuku ambapo vina vya ushairi vitaibua wazo badala ya wazo kuibua vina. Mnyampala anasisitiza kwamba washairi wenzake watumie mtindo huu ili waibue msamiati mbalimbali unaoweza kutumika kukuza Kiswahili.

Mbinu hii imejitokeza katika mashairi mbalimbali yaliyomo katika diwani hiyo. Baadhi ya mashairi hayo ni "Hima Hima Islamu" (uk. 6), "Mali Pepo Dunia" (uk. 7), "Fadhili Zao Tulipe"(uk. 7), "Heri Mwenye Sura Mbaya" (uk. 8), "Wastara Hazumbuki" (uk. 9), "Urafiki Tufanane" (uk. 11) na "Simbiko Haisimbiki" (uk. 13). Mbinu hii ya kiuandishi imejitokeza pia katika baadhi ya beti zilizomo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*. Kwa mfano, katika shairi la "Saba-Saba", ubeti wa pili (uk. 3) umetumia mbinu hiyo. Vilevile, mbinu hii imejitokeza pia katika shairi la "Kitung'ati" (uk. 7). Pia, imejitokeza katika *Waadhi wa Ushairi* katika shairi la "Mtambuzi" (uk. 20) na "Chambo" (uk. 32). Aidha, mtindo huu bado unatumiwa na baadhi ya waandishi wa ushairi wa Kiswahili katika karne ya 21, mfano mzuri ni mashairi ya Asha S.K. Kunemah (2008). Baadhi ya mashairi yake yanatumia mbinu hii katika utangulizi wake (rejea kitabu chake cha *Misemo na Methali katika Ushairi*, katika "Utangulizi" uk. 1, ubeti wa pili hadi wa tano na shairi la "Akili Nywele Kila Mtu ana Zake" uk. 45). Hivyo, inaonesha kuwa hadi sasa mtindo huu bado unatumiwa na baadhi ya watunzi ambao wanatunga kazi zao kwa kutumia mtindo wa kimapokeo.

[2] Mfano wa mashairi ya mtindo huu wa mtiririko umeambatishwa kwenye makala hii.

**2.1.2 Msisitizo**

Mtindo mwingine ambao uliibuliwa na Mnyampala ni mashairi ya msisitizo. Huu ni mtindo wa utunzi ambao aliuanzisha miaka ya 1960 na kuutumia kwa mara ya kwanza katika *Diwani ya Mnyampala* (1965) na *Waadhi wa Ushairi* (1965). Katika mtindo huu kila ubeti ulikuwa na kipande cha kusisitiza maudhui yaliyotengwa katika ubeti huo.[3] Mtindo huu ulitumiwa katika *Diwani ya Mnyampala* (kur. 121-130). Mfano shairi la "Natunga Msisitizo" (uk. 121) ubeti wa kwanza unasema hivi:

> Nawapangia maneno, ya sifa na walekezo,
> Na kuzitoa mifano, zinase nyoyo mawazo,
> Usemi wa sisitizo;
> Sisitizo mlingano, usioleta mivizo,
> Maagizo yawe **manono**, nayatilia mkazo,
> Natunga msisitizo, tungo zenye mwendo mpya.

Dondoo hilo linadhihirisha kuwa ubeti huu ulikuwa na mistari mitano na nusu. Kipande cha mstari kwa kila ubeti kilitumika kusisitiza maudhui ya ubeti husika. Mfano, katika ubeti huo maudhui kuhusu mtindo wa msisitizo yanapatikana katika kipande kisemacho 'usemi wa sisitizo.' Vilevile, Mnyampala alitumia mtindo huu katika *Waadhi wa Ushairi*, shairi la "Mambo Yanazidiana" (uk. 77). Licha ya mtindo huu kuwa mpya, ulifuata kaida za wanamapokeo ambazo ni matumizi ya urari wa vina na mizani kama uti wa mgongo wa ushairi wa Kiswahili.

Mtindo wa msisitizo kwa bahati mbaya haukupata kuenea na kutumiwa na watunzi wengine. Huenda haukuenea kwa kuwa watunzi na waimbaji wengi wa mashairi ya Kiswahili kwa wakati huo walikuwa wamezoea mtindo uliokuwapo wa mashairi ya kimapokeo yenye mistari minne (tarbia). Pia, mtindo huu unahitaji mtu ambaye ni mahiri katika uteuzi wa maneno na mwenye ubunifu wa kiwango cha juu katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Isitoshe, kutotumika kwa mtindo huu huenda kumesababishwa na kukosekana kwa utafiti wa kina kuhusu Mathias Mnyampala, hivyo, kusababisha kutofahamika kwa mtindo huo kwa waandishi chipukizi. Kwa hiyo, kupitia utafiti huu mtindo huu unaweza kupata watumiaji katika utunzi wa kazi za ushairi.

Kwa ujumla, mtindo huu ni mwafaka na unafaa kutumika katika ushairi wa Kiswahili. Mtindo huu unaleta mvuto katika sanaa ya ushairi na kumfanya msomaji kuwa na hamu ya kujua maudhui yaliyomo katika ushairi husika. Kadhalika, mtindo huu ulisaidia kuleta upya katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Mtindo huu licha ya kuasiliwa kwa kufuata urari wa vina na mizani kwa namna fulani, ulileta mabadiliko katika umbo la sanaa ya ushairi kwa kuwa umbo lililokuwa limezoeleka wakati huo lilikuwa ni la ubeti wenye mistari minne au

[3] Maelezo haya nimeyatoa katika dibaji ya *Maisha ni Kugharimia* iliyoandikwa na Charles Mnyampala (mtoto wa Mathias Mnyampala). Kadhalika, mfano wa mtindo wa mashairi haya umeambatishwa kwenye makala hii.

mitano. Mnyampala aliibuka na mtindo mpya kutokana na mtindo uliokuwapo. Kama asemavyo Eliot (1988), mshairi huathiriwa na watunzi wengine kiutunzi na kuibuka na kitu kipya ambacho kinatosheleza wakati huo. Hivyo, Mnyampala aliibuka na umbo lenye mistari mitano na nusu. Hii inaonesha kuwa Mnyampala alikuwa mbunifu na alipenda mabadiliko katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili.

### 2.1.3 Majibizano

Mnyampala alifufua mtindo wa majibizano baina ya wahusika wawili au zaidi katika mashairi yajulikanao kama ngonjera. Mmbaga (2004) anaeleza kuwa ngonjera zimetungwa kwa kutumia mtindo wa tarbia ambao kihistoria zilikuwapo nyakati za Muyaka bin Haji katika karne ya 18, kabla hata ya Mnyampala kuanza kuzitunga. Ngonjera hizo hazikuwa na sura ama mtindo huu tunaouona katika ngonjera za Mnyampala ambazo zinapatikana katika vitabu vyake vya *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2* (Mmbaga, 2004 na Mulokozi, 2017). Mulokozi (2017) anaeleza kuwa kabla ya Mnyampala, ulikuwapo ushairi wa majibizano, lakini ushairi huo haukuwa wa maigizo kwa namna ya kingonjera, bali ulikuwa unatambwa tu kwa kujibizana kati ya wahusika au watu wawili au pande mbili zenye kushindana mfano katika ngoma na shughuli za arusi. Anafafanua zaidi kuwa wahusika waliokuwa wanajibizana walikuwa wanajitungia maneno yao wenyewe. Walikuwa hawapokezani kama shairi au wimbo uleule na majibizano hayo yalikuwapo na bado yapo Ugogoni, Uswahilini na katika makabila mengineyo.

Hivyo, kutokana na maelezo ya Mulokozi ni dhahiri kuwa Mnyampala aliathiriwa na fasihi simulizi ya kabila lake la Kigogo. Mnyampala alichukua majibizano yaliyokuwapo katika fasihi simulizi ya kabila lake na ubunifu alioupata kutoka katika maandishi ya watu wengine na kuunda ushairi wa majibizano (ngonjera) wenye kuigizika. Kazi teule za Mnyampala zina majibizano ya aina mbili; majibizano ya papo kwa papo ndani ya shairi moja na majibizano kati ya mshairi mmoja na mshairi mwingine. Mfano wa majibizano ya papo kwa hapo yapo katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2*. Majibizano ya mshairi na mshairi yanapatikana pia katika *Diwani ya Mnyampala* (kur. 17-18); majibizano hayo ni baina ya Mnyampala na Snow White. Kama asemavyo Mnyampala katika diwani yake kuwa Snow White alipinga shairi lake la “Tusitukane Wakunga” (kur. 17-18) kupitia shairi lake la “Kuzaa si Kazi Kubwa, Kazi Kulea Mwana.” Mnyampala alimjibu tena katika shairi la “Tutalea Mwana Gani?” ambalo linapatikana katika diwani hiyo (uk. 18).

Utafiti huu umegundua kuwa Mnyampala ndiye aliyefufua na kuendeleza kwa kuweka mtindo huu kibunifu zaidi kiasi cha kuwafanya watafiti na wahakiki wengine kama vile Komba (1969) na Mwangomango (1971) wahisi kwamba ndiye aliyeanzisha ngonjera. Mnyampala aliweza kuchukua mtindo uliokuwapo na kuuboresha zaidi kulingana na muktadha wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea uliokuwapo wakati huo. Hivyo, mchango wake ni kuyafanya mashairi ya

majibizano yawe ya kimaigizo pamoja na kuyatafutia mashairi hayo kisawe chake (yaani akayapa jina la ngonjera). Ngonjera ni neno la asili ya Kigogo lenye maana kwenda pamoja; ni mashairi yaliyovuma sana wakati wa siasa za Ujamaa na yalianzishwa kwa lengo la kueneza siasa hizo. Katika kipindi hiki watu walitakiwa kuishi pamoja na kwa ushirikiano katika vijiji vya ujamaa ili waweze kujenga nchi na kufaidi matunda yake kwa pamoja. Majibizano yaliyokuwamo katika ngonjera hizo kwa kiasi kikubwa yamejengwa katika mfumo wa maswali na majibu. Mfano mzuri ni *Ngonjera za UKUTA Na. 1* ngonjera ya "Utukufu wa Taifa" (uk. 12) inayosema:

**Raia**
Bwana ninayo mashaka, makubwa yananitatiza
Nami sinayo hakika, lipi la kutanguliza
Jambo ninalolitaka, ni ninyi kunieleza
Lipi la kutanguliza, kwa taifa kulifanya?

**Mwanasiasa**
Maswali nimepulika, hayo uliyoniuliza
Kauli hajatamka, mbinu zake kueleza
Ni yapi unayotaka, pengine kutanguliza
Fumbua na kufumbuza, kwa taifa kulifanya

Kupitia majibizano hayo, Raia anamuuliza swali Mwanasiasa na Mwanasiasa anajibu. Katika majibizano hayo Mwanasiasa ndiye aliyepewa hadhi ya juu. Hapa inaonesha kuwa mwanasiasa ndiye anajua kila kitu na ndiye wa kuelimisha jamii. Wahusika hao wanaendelea na majibizano na mwishowe Raia anaonekana kuelewa maana ya kitu kinachozungumzwa. Raia alikuwa anaelezwa kuhusu utukufu wa taifa. Mwanasiasa anasisitiza kuwa kitu cha kutanguliza mbele ni kulijenga taifa, kuondokana na ukabila na udini na kutanguliza masilahi ya taifa. Utanzu huu wa ngonjera ulifufuliwa kwa kufanywa upya zaidi kimwingilianomatini na kutumiwa sana wakati wa siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Hivyo, watunzi wengi walihusisha ngonjera na masuala ya siasa yaliyokuwa yakiendelea nchini Tanzania katika kipindi hicho.

Utanzu huu ulitumiwa na baadhi ya watunzi wa mashairi waliotunga mashairi yao miaka ya 1970 hadi sasa. Mfano Kezilahabi (1974) katika diwani ya *Kichomi* (taz. kur. 51-58). Kezilahabi aliutumia mtindo huo kwa kutumia mashairi ya kisasa yasiyozingatia kanuni za ushairi wa kimapokeo. Hata hivyo, utanzu huu bado unatumika na wanafunzi wa shule za msingi (awali) na sekondari (upili) nchini Tanzania hasa katika mahafali na hata katika maadhimisho ya shughuli mbalimbali za kijamii na kisiasa. Kadhalika, mtindo wa majibizano unaendelea kutumiwa na washairi wa kimapokeo na kisasa wa karne ya 21 kama vile Kunemah (2008) katika diwani yake ya *Misemo na Methali katika Ushairi* (uk. 1). Majibizano yaliyotumika ni sawa na yale aliyokuwa anatumia Mnyampala katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*.

Kithaka wa Mberia naye anatumia majibizano katika diwani zake za ushairi, ijapokuwa hazingatii arudhi za ushairi wa kimapokeo. Suala hilo linajitokeza katika diwani ya *Mchezo wa Karata* (1997), katika shairi la "Kiwambo cha Televisheni" (kur. 37-39) na *Radio na Mwezi* (2005) katika shairi la sauti (kur. 61-63). Hata hivyo, Kithaka wa Mberia akiwa mtaalamu wa drama ameandika mtindo huo kwa kuzingatia mabadiliko yanayojitokeza katika jamii kwa kuboresha zaidi na kuuweka zaidi katika drama.

### 2.1.4 Vidato

Mtindo wa vidato ni ule ambao kuna kubadilishana kwa vina hatua kwa hatua ndani ya shairi moja. Katika mtindo huu vina vya mwisho vya mistari mitatu ya ubeti wa kwanza ndivyo vinakuwa vina vya kati vya mstari mitatu ya ubeti unaofuata na vina vya mwisho hutafutwa vingine. Hivyo, ubeti unaofuata unategemea vina vya kati kutoka katika ubeti uliotangulia[4]. Mbinu hii inajidhihirisha vyema katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*. Mnyampala (1966) anaeleza kuwa mtindo huu wa vidato ni aina fulani ya mashairi makuu kama yale mengine yaliyowahi kusifiwa ulimwenguni humu katika lugha mbalimbali za ulimwenguni, kama vile mashairi ya akina Shakespeare wa Uingereza, Mahabharata na Hamayana wa Bara Hindi la *Kale*, *Illiad* na *Odyssey*. Aidha, Mnyampala (1967) katika mswada wa *Hazina ya Washairi* anasema kuwa mtindo huu ulianzishwa katika mwaka wa 1966 na unafanana kidogo na ule uitwao "msisitizo" ambao unatokana na mawazo mazito na yenye hekima.

Naye Charles Mnyampala (2014) anaeleza kuwa Mnyampala ndiye aliyeanzisha mtindo wa mashairi ya vidato. Aidha, katika mahojiano yetu na Madumulla anafafanua kuwa mtindo wa mashairi ya vidato haukuanzishwa na Mnyampala bali aliuendeleza kutoka kwa washairi waliotangulia kama vile Muyaka bin Haji ambaye aliishi kati ya mwaka 1776 na 1840 na wengineo[5]. Tumepitia *Diwani ya Muyaka* na kubaini kuwa ni kweli mtindo huo ulikuwapo tangu enzi za Muyaka bin Haji. Rejea shairi la "Uaminifu" (uk. 1) na shairi la "Umwongo" (uk. 92). Hivyo, mtindo huu umetumiwa na Mnyampala katika kutunga mashairi yote yaliyomo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*. Mfano shairi la "Uaminifu" (uk. 1) ubeti wa pili na wa tatu zinasema:

Simama kadamnasi, ubaya ujitakase,
Ujitape ufarisi, wasikizi uwanase,
Kama mtu Ibilisi, watu budi wakususe,
Japo tusi usiguse, haja kubwa waminifu.

Mke mwema usikose, mtii mwenye hekima,

[4] Mfano wa mashairi ya mtindo wa vidato umeambatishwa kwenye makala hii.
[5] Maelezo haya yalitolewa na Profesa Joshua Madumulla katika Chuo Kikuu cha Iringa tarehe 14/10/2016.

Na amri afuase, akulee kama mama,
Kama macho apepese, huko afanye dhuluma,
Japo unatunzwa vema, haja kubwa waminifu.

Katika beti hizo vina vya mwisho ubeti wa pili vya mistari mitatu ya mwanzo ambavyo ni "se" vimekuwa vina vya kati vya ubeti wa tatu katika mistari mitatu ya mwanzo. Kadhalika, ubeti wa nne, vina vya mwisho vya mistari mitatu ya mwanzo vya ubeti wa tatu "ma" ndivyo vimetumika kuwa vina vya kati vya ubeti wa nne. Hivyo, kila ubeti unaofuata unachukua vina kutoka ubeti tangulizi. Katika mtindo huu wa vidato kuna mwingiliano wa vina kama tulivyoonesha hapo juu. Hata hivyo, si mwingiliano wa vina tu, pia kuna mwingiliano wa maudhui yaliyomo ndani ya shairi husika. Vilevile, kuna mwingiliano wa mbinu hiyo kutoka kwa watunzi watangulizi kama tulivyoeleza hapo awali.

Makaka (2012) anaeleza kuwa mnamo mwaka wa 1966 Mnyampala alikuwa mhadhiri wa muda mfupi wa fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mojawapo ya kozi zilizofundishwa wakati huo ilikuwa ni mashairi ya Kiswahili. Anaongezea kuwa wanafunzi wa Kiswahili katika Chuo hicho walijifunza na kujadili mashairi ya Sayyid Abdala bin Ali Nassir, Muyaka bin Haji na ya Sheikh Amri Abedi[6]. Ni dhahiri kwamba Mnyampala aliyajua vizuri mashairi ya watangulizi wake kama ilivyoelezwa hapo awali. Ufahamu wake ulimfanya afufue na kuendeleza mbinu hiyo, na kuutafutia kisawe chake. Kwa upande mwingine, inawezekana kwamba Mnyampala aliandika pasipo na kufahamu kuwa Muyaka naye alitumia mtindo huu. Hata hivyo, Mnyampala alikuwa mdadisi, mtu aliyependa kujifunza na kuona wengine wanafanyaje ili kuweza kuibua mitindo mipya ama kuiendeleza mitindo ambayo ilionekana ni mizuri lakini imeanza kutoweka katika jamii. Kwa kufanya hivyo, Mnyampala alijitahidi kuleta mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili na kuyafanya mashairi yake kuwa na upekee wa namna yake.

Aidha, Mnyampala alijitahidi kutunga mashairi yake kwa kuteua maneno mazuri na yenye maana kulingana na ujumbe anaotaka kuwasilisha katika jamii. Pia, alikuwa na ufanisi mkubwa wa kupanga vituo na vina vinavyowiana vizuri ili mashairi yake yakiimbwa yapendeze masikioni mwa wasikilizaji. Kwa ujumla, Mnyampala alikuwa mshairi mwenye ujuzi wa lugha na mwenye kupenda mabadiliko katika ushairi wa Kiswahili. Hamu yake ilikuwa kutaka sanaa ya ushairi iendelee mbele, ndiyo maana alijitahidi kuibua mitindo mipya na kufufua mitindo mbalimbali katika utanzu huu. Naye Williams (1974) anaeleza kuwa mtindo wa mashairi mengi ya Mnyampala ni wa kimapinduzi, unaobadilikabadilika na unaoleta mabadiliko makubwa katika ushairi wa Kiswahili kutokana na mashairi ya kimapokeo ya akina Akilimali na wenzake. Tunaweza kusema kuwa Mnyampala alithubutu kuleta mabadiliko katika ushairi

[6] Taarifa hizi pia tulizipata katika mahojiano na nyaraka zake zilizohifadhiwa nyumbani kwake. Baadhi ya nyaraka zinazothibitisha hilo tumeziambatisha kwenye makala hii.

wa Kiswahili kwa kubuni mitindo mipya ya uandishi na kufufua mitindo iliyoonekana kusahaulika kwa kuweka ubunifu zaidi na kuzifanya baadhi ya tungo zake zionekane kama mpya. Bila shaka mtazamo huu wa Mnyampala ndio uliosababisha hata watunzi wengine kufikiria kuleta mabadiliko katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili na fasihi kwa ujumla. Hivyo, kutokana na mabadiliko aliyochangia katika ushairi, kazi zake ni kielelezo kizuri cha Nadharia ya Urasmi Mpya katika fasihi ya Kiswahili.

**2.2 Muundo**

Dhana ya muundo katika shairi imezungumziwa na watu mbalimbali. Miongoni mwa waliojadili muundo ni Mulokozi (2017) anayefafanua kuwa miundo ya ushairi wa Kiswahili ni mingi. Mashairi yana miundo mbalimbali kutegemea ufundi wa mshairi mwenyewe. Mulokozi anabainisha baadhi ya vipengele vinavyotumika zaidi katika muundo wa ushairi kuwa ni mistari, beti, mizani na vina. Mulokozi anaeleza kuwa katika ushairi kuna muundo ndani (maudhui) na muundo nje (fani). Kwa ujumla, muundo ndani na muundo nje huhusiana na kukamilishana. Katika mashairi ya kimapokeo wanazingatia zaidi mgawo wa vipande, idadi ya mistari katika kila ubeti, kiitikio au mkarara au kibwagizo na idadi ya beti katika shairi (Samwel na wenzake, 2013).

Mnyampala ametumia miundo mbalimbali katika uandishi wa kazi zake za ushairi. Uandishi wa mashairi ya Mnyampala, muundo wa tarbia (mistari minne kila ubeti) ndio umetamalaki katika kazi zake. Kadhalika, yapo mashairi yenye ubeti mmoja tu, rejea *Waadhi wa Ushairi* (uk. 1-6 na 7-11) na kuna mashairi yenye beti mbili (uk. 7-11). Vilevile, katika diwani hiyo kuna mashairi yenye muundo wa beti tatu (uk 11-16), na beti nne (uk 17-18), tano (uk. 33-47), sita (uk. 48-54), saba (uk. 55-61), tisa (uk. 62-65), kumi (uk. 65-78), kumi na moja (uk. 78-80) hadi beti kumi na mbili (uk. 80-84) na mwisho kuna utenzi wa "Kifo cha Mama" na "Mawaidha" (uk. 85-86). Mashairi hayo ameyapanga kwa mpangilio akianza na yenye beti chache na kuelekea yenye beti nyingi. Pia, muundo wa Mnyampala unabadilikabadilika, kwa mfano, katika dibaji ya *Waadhi wa Ushairi* ametumia mashairi yenye mistari mitatu (tathilitha) (taz. kur. x-xi), mfano wa shairi mojawapo ni hili:

> Chungu cha Johari kito, Kinivemeto na moyo!
> Shirabu yako ya mato, inisayo wayo wayo,
> Laiti nisiwe mto, hakinga matozi hayo? (kur. x-xi)

Mashairi mengi zaidi katika kazi zake ni yale yenye mistari minne. Vilevile, ushairi wa Mnyampala una muundo wa mashairi yenye mistari sita ama mitano na nusu, ambayo ameyaita mashairi ya msisitizo ambayo yanapatikana pia katika *Waadhi wa Ushairi* na *Diwani ya Mnyampala*. Katika *Diwani ya Mnyampala*, mashairi haya yanapatikana kuanzia shairi la "Natunga Msisitizo" (kur. 121-130). Muundo huu wa msisitizo pia umo katika *Waadhi wa Ushairi*, shairi la "Mambo

Yanazidiana" (kur. 77-78). Kwa ujumla, Mnyampala katika mashairi yake hayo ya tathlitha na tarbia huwa mistari yake imegawanyika katika vipande viwili ambavyo huwa na mizani kumi na sita, kila kipande huwa na mizani nane. Aidha, shairi la "Kifo cha Mama" na "Mawaidha" (kur. 78-79), ametumia muundo wa tenzi, ambao ubeti huwa na mistari minne yenye mizani nane kwa kila mstari. Shairi hilo la "Kifo cha Mama" (uk. 78) linaonekana hivi:

Kifo kwetu ni faradhi,
Kuletwako na maradhi,
Japo kifo chatuudhi,
Wapi tutakimbilia?

Kweli dunia ni pana,
Viumbe twazaliana,
Sivyo tungekanyagana
Twazaliwa twapungua.

Nukuu hapo juu inaonesha kuwa kila ubeti una kibwagizo chake. Pia, kuna mashairi mengine ambayo kibwagizo hubadilishwa katika kila kipande cha mstari, mfano shairi la "Uaminifu" (uk. 1) na "Kiasi" (uk. 4) katika *Mashairi ya Vidato*. Hivyo, Mnyampala aliweza kutumia miundo inayobadilikabadilika katika kazi zake za ushairi. Tunaweza kusema kuwa mabadiliko katika umbo la ushairi yalianza taratibu na baadhi ya wataalamu wa ushairi wa kimapokeo, akiwamo Mnyampala, alikuwa mstari wa mbele katika kubadili miundo ya mashairi yake na kuleta upya katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili.

Kwa ujumla, miundo aliyotumia Mnyampala ina mchango katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili na inatumika hadi sasa na baadhi ya waandishi wa karne ya ishirini na moja, kwa mfano, mashairi ya Kunemah (2008) na Walibora (2007). Hivyo, ni dhahiri kuwa mchango wa washairi wa kimapokeo ni muhimu katika kuendeleza ushairi wa kisasa. Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa muundo wa shairi lazima uamuliwe na kufungamana na mawazo, mtiririko wa hisia na makusudio ya mtunzi. Kwa hiyo, mtunzi yeyote ni lazima aongozwe na maudhui, hisia na makusudio ya utunzi.

Mnyampala alikuwa mbunifu na mahiri katika kutumia miundo mbalimbali. Aliweza kutumia muundo wa kipande, msitari na ubeti mmoja kuwasilisha ujumbe unaojitosheleza kwa walengwa. Miundo ya Mnyampala katika ushairi wa Kiswahili inaonesha ukomavu katika mbinu za utunzi na ujuzi wa lugha ya Kiswahili. Kupitia miundo yake aliweza kuibua misamiati na kukuza lugha ya Kiswahili. Mchango wa Mnyampala katika muundo wa shairi wa Kiswahili hauna kifani.

### 3.0 Maudhui

Maudhui hujumuisha mawazo na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mtunzi ama msanii kutunga kazi ya fasihi. Mulokozi (2017) anaeleza kwamba maudhui ni

mawazo au mambo yanayosemwa ndani ya kazi ya sanaa. Mulokozi anafafanua kuwa kila shairi husema kitu fulani, na hukisema kwa mtazamo fulani ili kutimiza lengo fulani. Anaongezea kuwa mada inayozungumziwa na shairi huitwa dhamira. Dhamira inapounganishwa na mtazamo wa mtunzi, shabaha, ujumbe, muktadha, tunapata maudhui ya shairi linalohusika. Hivyo, maudhui yanajumuisha dhamira, ujumbe, migogoro, falsafa na msimamo au mtazamo. Kwa ujumla, maudhui yanaweza kuhusu jambo lolote linalomkera ama kumsumbua mwanadamu, kwa mfano maana ya maisha, mapenzi, siasa, mauti, ndoa, elimu, kazi, ukombozi na dini. Yote hayo yanajitokeza kwenye kazi za Mnyampala kama ilivyo kwa watunzi wengine. Kwa upekee, Mnyampala ameweza kuingiza masuala ya dini katika ushairi wa Kiswahili.

### 3.1 Maudhui ya Dini katika Ushairi wa Kiswahili

Mnyampala ambaye alikuwa Mkristo wa kwanza kutunga na kuandika mashairi ya Kiswahili, alisaidia kuelimisha jamii kuwa ushairi wa Kiswahili si kwa ajili ya Waislamu tu. Hivyo, alitoa mwelekeo mpya kwa kuonesha kuwa ushairi pia huweza kutungwa kwa kuhusisha maudhui ya Kikristo kupitia kazi zake na kuchangia kukuza taaluma ya ushairi. Mnyampala alisaidia kusawiri Ukristo katika kazi za ushairi kupitia kazi zake za *Utenzi wa Injili* na *Utenzi wa Zaburi*. Vilevile, katika *Diwani ya Mnyampala* kuna shairi la "Kiongozi Mtukufu" (uk. 26), "Rabbi Yesu Kazaliwa" (uk. 39) na "Amezaliwa Mwokozi" (uk. 130).

Kadhalika, Mnyampala katika kazi zingine za ushairi aliingiza maudhui ya dini zote mbili ya Kikristo na Kiislamu (Kyamba, 2018). Hii inaonesha kuwa Mnyampala hakuwa mbaguzi wa dini. Hata hivyo, huenda mawazo ya Mnyampala ya kuweka maudhui yahusuyo Ukristo katika ushairi yalitokana na waandishi wa karne ya kumi na nane na kumi na tisa. Tungo zinazohusu maudhui ya dini ya Kiislamu kama vile *Utenzi wa Al-Inkishafi* uliotungwa na Sayyid Abdallah Bin Ali (1810), *Utenzi wa Hamziya* uliotungwa na Seyyid Aidamis bin Athuman (1749) na *Diwani ya Muyaka* bin Haji Al-Ghassaniy ambaye inasadikika aliishi miaka ya 1776-1840 (Bhalo, 1977; Shitemi, 2010) na nyinginezo zilizohusu maudhui ya Kiislamu.

Aidha, waandishi wengine mashuhuri wa karne ya ishirini kama vile Shaaban Robert, Amri Abedi, Saadani Kandoro, Mahmoud Hamdouniy, Akilimali Snow White walitumia sanaa ya ushairi kutoa mawaidha ya dini ya Kiislamu katika baadhi ya beti za mashairi yao. Kwa mujibu wa Ponera (2010), Shaaban Robert ni mshairi aliyetumia sanaa ya ushairi kutoa maadili ya kidini, mfano *Utenzi wa Hati* (kur. 8-22) na *Utenzi wa Adili* (kur. 23-40) ambazo zinapatikana katika kitabu cha *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1991). Katika tenzi hizo aliwataka wanawe Mwanjaa na Selemani wafuate maadili na kushika dini, kuwa wasafi kiroho na kuachana na anasa za dunia. Shaaban Robert aliwausia wanawe wamtangulize Mungu katika yote na kushika dini, hususani dini ya Kiislamu. Hapa tunaweza kusema kuwa Shaaban Robert katika utunzi wake

alitunga akiegemea zaidi katika dini ya Kiislamu. Kwa upande wa Muyaka, baadhi ya mashairi yake yalihusu dini ya Kiislamu, lakini Mnyampala alitunga mashairi yake kwa kuunganisha dini zote mbili, Ukristo na Uislamu. Hivyo, tunaweza kusema Mnyampala alikwenda mbele zaidi kwa kuchanganya dini zote mbili katika utunzi wake. Vilevile, Mnyampala (2011:9) anamwelezea Amri Abedi kuwa ni "mshairi aliyetumia sanaa yake kutoa mawaidha kuhusu dini ya Kiislamu," mfano katika ubeti wa kumi, na ubeti wa kumi na mbili anasema:

> Dini hukuipokea, ninashukuru Mola,
> Kamilisha dini pia, kwa kutabii Rasula,
> Mshenga kutufikia, hazitatufaa hila,
> Dawa mziwanda kula, kula upate afia.
>
> Rahimu Mola Jalia, ninashukuru Allah,
> Mara kwa mara jalia, nandika hizi risala,
> Mshairi aje jua, Mjumbeo wa fadhila,
> Dawa mziwanda kula, kula upate afia.

Mnyampala anaeleza kuwa shairi hilo lilitungwa kwa ajili ya kumhubiria dini mpwawe bwana Saadani Abdu Kandoro ili afuate madhehebu ya Ahmadiyya. Shairi hili linapatikana pia katika kitabu cha *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Kwa ujumla, mashairi hayo yalikuwa yanahusu maudhui ya dini ya Kiislamu. Kutokana na mwelekeo huo, katika utafiti huu tumebaini kwamba Mnyampala naye aliona kuna umuhimu wa kutumia sanaa ya ushairi kutoa mawaidha ya dini ya Kikristo. Mnyampala alikuwa Mkristo wa kwanza katika uandishi wa ushairi na aliyeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mafundisho ya Kikristo na mwalimu wake Damiani[7]. Hivyo basi, Mnyampala alijitahidi kuonesha kuwa ushairi si kwa ajili ya Waislamu tu bali unafaa pia kupitisha maudhui ya Kikristo na kipindi hicho washairi Wakristo walikuwa Mnyampala na Nyerere. Vilevile, kuna mashairi ya Mnyampala yanayohusu dini ya Kikristo na Kiislamu yanajitokeza vyema katika *Diwani ya Mnyampala* (Kyamba, 2018). Pia, uhusiano wa Mnyampala na dini nyingine unaelezwa vyema katika historia ya maisha ya mwandishi (Kyamba, 2018).

Aidha, katika mswada wa *Fasili Johari ya Kiswahili*, Mnyampala (1959) anatoa maelezo yanayohusiana na matumizi ya ushairi katika Maandishi Matakatifu. Hii inatuthibitishia kuwa Mnyampala alisoma na kuelewa vizuri Maandishi Matakatifu. Aliweza kugundua sehemu mbalimbali za *Biblia Takatifu* na *Kurani Tukufu* zinazozingatia kanuni ya arudhi ya ushairi. Kwa ujumla, Mnyampala alikuwa mshairi mdadisi ndiyo maana aliweza kutambua jinsi ushairi ulivyotumika katika *Biblia Takatifu* na *Kurani Tukufu*. Mfano, katika (uk. 3) wa mswada wa *Fasili Johari ya Kiswahili*, anaeleza:

---

[7] Jina la Damiani limetumika hilo tu moja katika kitabu chake cha *Maisha ni Kugharimia* na maandishi yake mengine.

> Yumkini hapana cha kupungua juu ya kusudi la kuheshimu kazi ya mashairi na watunzi wenyewe. Utunzi au wimbaji wake haukuachwa, na matumizi ya mashairi yaliendelea kukua zaidi na zaidi kwa kufuata ushairi kuwa ni zana za shughuli za mahubiri ya dini. Hivyo, mashairi yalitumiwa pia katika enzi za maagano mapya.

Kutokana na maelezo hayo, Mnyampala alikuwa akizungumzia mahubiri na mafunzo ya dini zote katika ushairi wa Kiswahili, bila kujali tofauti za dini. Aidha, umoja wa watunzi unajibainisha hata katika kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* ambapo waandishi wa dini mbalimbali walionesha kushirikiana bila hata ya kuzingatia tofauti zao za kidini. Hivyo, Mnyampala na watunzi wengine walikuwa na umoja bila kujali tofauti za dini zao; walizingatia usawa wa binadamu na kuheshimu dini ya kila mmoja. Mashairi ya Mnyampala yalihubiri upendo wa Mungu kwa watu wote.

Mshairi mwingine wa kipindi hicho Mkristo aliyetunga mashairi yenye maudhui ya dini ya Kikristo ni Nyerere aliyetunga tenzi tano, ambazo ni *Injili ya Matayo* (1996), *Injili ya Yohana* (1996), *Injili ya Marko* (1996), *Injili ya Luka* (1996) na *Utenzi wa Matendo ya Mitume* (1996). Kwa ujumla, tungo hizo zilieleza maisha ya Yesu na mafundisho yake hapa duniani kama ilivyokuwa katika tungo za Mnyampala hususani *Utenzi wa Injili* (1966). Washairi wengine ambao ni Wakristo katika ushairi wa Kiswahili walioibuka baadaye, hususani wanausasa, baadhi yao ni Euphrase Kezilahabi, Ken Walibora na Kithaka wa Mberia.

## 4.0 Mchango Mwingine wa Mashairi ya Mnyampala

Mbali na vipengele vya fani na maudhui tulivyoviangazia hapo awali, mashairi ya Mnyampala pia yana mchango katika kukuza nadharia ya Ushairi wa Kiswahili na kuweka pamoja aina mbalimbali za mashairi. Tumefafanua zaidi mchango huo katika vipengele viwili vinavyofuata hapa chini.

### 4.1 Kukuza Nadharia ya Ushairi wa Kiswahili

Wafula na Njogu (2007) wanaifasili nadharia kama miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya kifasihi kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Fasili hii, zaidi ya ubora wake, ina udhaifu mkuu mmoja wa kuchukulia kwamba kazi ya fasihi lazima iwe andishi, kumbe kazi ya fasihi inaweza pia kuwa simulizi. Wamitila (2003) anasema kwamba nadharia ni sayansi au sanaa inayohusika na kanuni za kijumla na mikabala au hata kanuni fulani zinazotumika katika uchanganuzi wa suala fulani. Aidha, tunaweza kusema kuwa nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo, imani au mkabala fulani wa mawazo ya watu fulani juu ya jambo fulani. Kadhalika, nadharia inaweza kutokana na mawazo yaliyoundwa kitambo na jopo la wataalamu au inaweza kutokana na usomaji au usikilizaji makini wa kazi ya fasihi ya mtu binafsi. Kwa ujumla, maisha ya mwanadamu yanaongozwa na nadharia kadha wa kadha.

Kutokana na maana zinazohusu nadharia, katika utafiti huu tumebaini kuwa Mnyampala alikuwa na mwongozo aliokuwa anafuata katika utunzi wa mashairi yake. Kwa ujumla, mtunzi huyu alikuwa anafuata kaida za kimapokeo lakini umapokeo wake ulikuwa na mabadiliko fulani katika utunzi wake. Hivyo, alikuwa na nadharia yake ya kimapokeo iliyokuwa ikimwongoza katika utunzi wa kazi zake. Hili linajibainisha kwa kuangalia kazi zake kuhusu ushairi wa Kiswahili. Aidha, Mnyampala ni miongoni mwa wataalamu waliotoa maana ya ushairi pamoja na aina zake. Maana hiyo pamoja na aina za mashairi zinapatikana katika Dibaji yake ya *Diwani ya Mnyampala*. Anaeleza:

> Ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalumu kwa shairi. Shairi laweza kumliza mtu akatokwa na machozi kwa ajili ya mchomo wa hanjari la kuukata moyo na maini kwa ule mchomo na mguso wa maneno ya shairi la mshairi bora. Vilevile, shairi jingine laweza kuuburudisha moyo mtu akafurahi akthari ya furaha na kujiona kuwa nayo heri mithili ya mtu aliye peponi. Shairi lina usemi ulio mtamu sana. Kwa maoni yanayopenya moyo yaliyo bora sana. Hivyo, ushairi una sifa iliyo bora sana ulimwenguni na mafunzo yenye uadilifu na mazingira ya dunia yalivyo (Mnyampala, 2014: vii).

Kutokana na dondoo hili, tunapata wazo kuwa kwa mujibu wa Mathias Mnyampala miongoni mwa sifa za ushairi wa Kiswahili ni kutumia lugha ya kishairi isiyokuwa na maneno ya kashfa wala matusi. Pia, ushairi unapaswa kuwa na urari wa vina na mizani kamili zinazotakiwa katika ushairi wa Kiswahili. Sifa nyingine za ushairi wa Kiswahili anazobainisha mtunzi huyu ni kuwa shairi linapaswa liwe na vina vinavyopatana au vinavyolingana, hususani mwishoni mwa kila mstari kwa ubeti mzima, ingawa vina vya kati vinaweza kukosekana. Katika dibaji hiyo, Mnyampala anasisitiza juu ya sanaa ya shairi kwa kusema kuwa shairi la Kiswahili lihusu mwendo wa mashairi bora, yaani linatakiwa lisizidi mno maneno ya kurudiarudia, lisitungwe namna ya kulinganisha matuta, lisiwe pyororo (lisiloeleweka) bali liwe shairi kamili kama mashairi ya watu mahiri, werevu na wenye hekima. Mnyampala alichangia katika kutoa maana ya ushairi kwa kuegemea katika mkondo wa wanamapokeo. Kwa kufanya hivyo amechangia kukua kwa nadharia ya ushairi wa kimapokeo.

Mnyampala alikuwa miongoni mwa wataalamu wa mwanzo kutoa aina za ushairi. Mnyampala aliweza kutoa aina tano za ushairi: "mashairi ya kawaida, mashairi ya furaha, mashairi ya huzuni, mashairi mazito na mashairi ya kuadibu" (taz. *Diwani ya Mnyampala*, 2014:vii-viii). Kila aina ya ushairi ina vipera vyake vifuatavyo: kwa mfano, "mashairi ya kawaida" vipera vyake ni: mawaidha ya dunia, visa na mikasa kwa kawaida, wasifu wa kila kitu kwa ujumla, furaha au huzuni na shairi maalumu. "Mashairi ya furaha" yana vipera hivi: kushangilia

tamasha, kutakia kheri na mafanikio, wasifu wa furaha hiyo ilivyo, ombi la kudumisha furaha hiyi, na waadhi kwa ajili ya tafrija hiyo. Pia, "mashairi ya huzuni" yana vipera kama: shairi la rambirambi (kama ni kifo), maombezi kwa Mungu kwa ajili ya marehemu, maombezi kwa wale waliobaki wanaomhusu, historia marehemu (kama inajulikana), kumbukumbu itakiwayo, shairi la tanibihi na stighifari, shairi la manusurina, shairi la pole yenyewe iliyomfika mtu, kumtahadharisha ya mbele na uzindushi wa jumla. Vilevile, "mashairi mazito" yanaundwa na vipera vifuatavyo: shairi la kuzama (kufumba), shairi la tambo (kutega fumbo), pigo kuu la ushairi na taaluma zake, fahari ya ushairi na taaluma zake na kuonesha mbinu za lugha ya mshairi yule. Kadhalika "mashairi ya kuadibu" vipera vyake ni: kumuonya mtu kinaganaga bila kutumia utusi, kumtanabahisha ya hatima, ni nini hasara ya upujufu, uungwana ni nini na Maandiko Matakatifu.

Aina hizi za ushairi zilizoainishwa na Mnyampala ni mchango wake mmojawapo katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mbali na aina hizi za ushairi, mtunzi huyu amependekeza sheria za ushairi ambazo hazifai tu kwa ushairi wa kimapokeo bali pia hata katika ushairi wa kisasa kama alivyofanya Amri Abedi (1954). Tunazipata sheria hizi katika Dibaji ya *Diwani ya Mnyampala*, Mnyampala anaeleza kuwa washairi hodari hutunga mashairi yao kwa nadhari[8] za aina tano (kur. viii-x), ambazo ni:

Mosi, shairi liwe na *poetical Swahili*[9], yaani Kiswahili kinachohusu mwenendo wa mashairi bora. Pili, shairi liwe na urari wa mizani kamili zinazohusika na ushairi wa kawaida kwa lugha ya Kiswahili kisichokuwa na kashfa ya utusi ndani yake. Tatu, shairi liwe na vina vinavyopatana, hususani mwishoni mwa kila ubeti kwa shairi lote zima ingawa vina vya katikati vikosane kwa utenzi wake. Nne, shairi kama halikulingana vina vyake, yaani mtiririko, lizingatie na muwala - liwe na maana iliyo bora sana yenye ufundisho ndani mwake, furahisho, mvuto wa maarifa ama kasida za kumsifu Mungu pengine watu maarufu na vitu vinginevyo vistahilio kusifiwa. Tano, lisizidi mno maneno ya kurudiarudia.

Kyamba (2016) anaeleza kuwa nadharia ya Mnyampala ya ushairi inahusu mashairi ya kijadi na maneno ya hekima. Pia, anasisitiza kuwa hata kama shairi halina vina basi liwe na mtiririko na muwala. Vilevile, kuwe na maana bora sana yenye mafundisho ndani mwake, ufurahisho, mvuto wa maarifa ama kasida za kumsifu Mungu, watu maarufu au vitu vinginevyo vinavyostahili kusifiwa. Kwa ujumla, nadharia ya Mnyampala ya ushairi wa Kiswahili ni muhimu sana katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa sababu Mnyampala ni miongoni mwa washairi wa kimapokeo waliosaidia kutoa maana ya ushairi, aina za ushairi,

---

[8] Ni kanuni, masharti au sheria.
[9] Linapatikana katika *Diwani ya Mnyampala*.

uundaji wa kanuni za ushairi wa kimapokeo pamoja na uundaji wa istilahi na msamiati mbalimbali wa ushairi na Kiswahili.

### 4.2 Kukusanya Mashairi ya Waandishi mbalimbali

Mnyampala aliweza kukusanya mashairi ya waandishi mbalimbali kwa lengo la kuyahifadhi kwa manufaa ya kizazi kijacho. Baadhi ya kazi alizokusanya na kuzihariri ni kitabu cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*, mswada wa *Hazina ya Washairi* na mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili*. Kukusanya mashairi mbalimbali na kuyaweka katika diwani moja kuliendeleza ushairi wa Kiswahili. Mashairi hayo aliyatoa katika magazeti mbalimbali mfano gazeti la *Mapenzi ya Mungu*, *Ngurumo* na *Mambo Leo* (Mnyampala, 1966 [Dibaji]). Mnyampala anaeleza kuwa kazi hiyo ya ukusanyaji wa mashairi mwanzoni ilifanywa na wageni, kama asemavyo mwenyewe katika dibaji yake ya mswada wa *Hazina ya Washairi* kuwa:

> Ukusanyaji wa mashairi ya washairi ilishughulikiwa hasa na wageni ambao hawakuwa wenyeji wa nchi hii-kama vile mashairi ya Fumo Liongo, mashairi ya Muyaka bin Haji Al-Ghassaniy, Utenzi wa Al-Akida, Utenzi wa Barasisi, Utenzi wa Mkonumbi na nyinginezo nyingi zilizokusanywa na wageni (uk. i).

Kutokana na nukuu hiyo tunabaini kuwa Mnyampala alipata wazo la kukusanya mashairi ya washairi wenzake kupitia washairi waliotangulia kama ionekanavyo katika dondoo hilo. Alinakiri mashairi ya washairi mabingwa na kuyaweka katika miswada kwa manufaa ya vizazi vijavyo kwa lengo la kujenga lugha ya taifa ambayo ni Kiswahili. Mashairi yaliyomo katika mswada wa *Hazina ya Washairi* yalianza kukusanywa mwaka 1965 (Mnyampala, 1966). Ukusanyaji wa mashairi hayo ulitokana na wito alioutoa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika utangulizi wa *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* kuwa waandishi wanatakiwa kuandika kitabu kingine kikubwa kuliko hicho. Mnyampala anabainisha hayo katika dibaji ya *Hazina ya Ushairi* akisema:

> Mawazo haya ya kukusanya mashairi yalikujaje? Nilikumbushwa na Mtukufu Raisi wetu Mwalimu Julius K. Nyerere wakati alipoandika utangulizi wa kitabu cha "Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi" kwa ajili ya toleo la pili, alisema: "Nawashukuru pia jamaa wa chama cha washairi kwa kukitoa kijitabu hiki. –Ninalowaomba zaidi ni kwamba wajitayarishe kututolea kijitabu kikubwa zaidi kuliko hiki" (uk. i).

Maneno hayo yalimpa Mnyampala hamasa ya kukusanya mashairi mengi zaidi ya tangu mwaka 1935 hadi 1965, ambapo alifanikiwa kwa kiasi kikubwa. Ukusanyaji huo una mchango mkubwa kwa maendeleo ya ushairi wa Kiswahili kwa kuwa tunapata kufahamu waandishi wengine walioandika kazi za ushairi wa Kiswahili. Pia, tunapata maudhui mbalimbali ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yaliyoibuliwa na waandishi hao.

Ukusanyaji wa mashairi ulifanywa pia na Saadan Kandoro ambaye aliandika kitabu cha *Mashairi ya Kandoro* (1972) chenye mashairi yake na mkusanyiko wa mashairi ya watunzi mbalimbali wa ushairi kama vile Julius Nyerere, Amri Abedi, Akilimali Snow White na wengineo. Vilevile, katika karne ya ishirini na moja tunaona waandishi kama vile Ken Walibora ambao wameweza kukusanya mashairi mbalimbali na kuhariri diwani iitwayo *Diwani ya Karne Mpya* (2007). Katika diwani hiyo kuna mashairi themanini yaliyotungwa na watunzi kumi na nane tofautitofauti wenye asili ya Kenya na Tanzania na wenye tajiriba ya maisha tofautitofauti ya ndani na nje ya Afrika Mashariki. Hivyo, katika mashairi hayo kuna mseto wa tajiriba, mikabala na mikondo mbalimbali. Mchanganyiko huo unachangia kuleta uhalisia pamoja na mwingiliano wa mambo katika nyanja mbalimbali za kisiasa, kijamii na hata kiuchumi.

Aidha, *Diwani ya Karne Mpya* imekusanya tungo za washairi wakongwe na wapya. Umuhimu wa diwani hii unadhihirika katika maudhui, mikabala ya kifalsafa, maumbo na miundo, pamoja na misisitizo ya washairi waliochangia mashairi. Haya yote yametokana na mchango wa waandishi waliotangulia akiwamo Mathias Mnyampala aliyewahi kukusanya mashairi ya washairi wengine na kuyahifadhi kwa manufaa ya taifa. Kama asemavyo Kezilahabi (1976), hamu ya kurejelea mbinu mbalimbali zilizotumika na washairi wa zamani zilichangia kuzua ushairi mpya. Maelezo ya Kezilahabi yanashadidia mawazo ya Wanamwingilianomatini wanaodai kuwa, hakuna kitu ambacho kinaibuka bila ya kutegemea mawazo ama matini zilizotangulia (Kristeva, 1981na Allen, 2000). Aidha, kazi za sanaa lazima ziwe na mwingiliano wa matini mbalimbali zinazoibua matini mpya inayoendana na muktadha husika.

Vilevile, Mnyampala aliweza kukusanya nyimbo mbalimbali maarufu kwa manufaa ya jamii na taifa kwa ujumla. Mswada wa *Mahadhi ya Kiswahili*, umesheheni nyimbo zilizokusanywa katika sehemu mbalimbali za Tanzania na pwani ya Kenya. Nyimbo hizo zilihusu kubembeleza watoto, jando, kutafuta mchumba na mahaba na mapenzi. *Mahadhi ya Kiswahili* ni mswada ambao haujachapishwa hadi sasa.[10] Aidha, maudhui yaliyomo katika mswada huu yanajitokeza pia katika nyimbo zinazotungwa katika karne hii za Hip Pop na Bongo Fleva. Hii inatuthibitishia kuwa fasihi inatokana na fasihi yenyewe na hakuna matini inayoibuka bila ya kutegemea matini tangulizi.

Sambamba na hilo, tumebaini kuwa baadhi ya nyimbo zinazopatikana katika mswada huu zilikuwa hazizingatii arudhi na idadi ya mistari hutofautiana kwa kila ubeti. Mtindo huo unajibainisha waziwazi katika nukuu hapa chini kutoka katika *Mahadhi ya Ushairi*:

Owani baba owani, kitunguu na ubani,

[10] Mswada huu wa *Mahadhi ya Kiswahili* niliupata nyumbani kwa mke wa Charles Mnyampala katika mahojiano yaliyofanyika Julai, 2016.

Nyoka kalala njiani, tumkanyage kichwani;
Usiache wenda kuni, na wendao kisimani,
Nitakupiga ukuni, uangukie majini,
Makosa niliyokosa, sina maombezi kwani?
Muombezi wangu nyota, na mwana wa Sultani,
Ooooh, mtoto, Oooo mtoto (uk. 2).

Katika nukuu hiyo, tumebaini kuwa wimbo si lazima uwe na mistari mitatu. Kwa mfano, wimbo huu una mistari saba na bado ni wimbo. Kadhalika, wimbo huu hauna urari wa vina katika vipande; mstari wa kwanza hadi wa nne vina vya kati ni ‘ni’ na mstari wa tano ni ‘sa’, ubeti wa sita ni ‘ta’ na ubeti wa saba ni ‘to’. Pia, katika ukurasa huohuo, kuna wimbo mwingine ambao hauzingatii urari wa vina, wimbo huo unasema:

Silie mama silie,
Ukilia waniliza, wanikumbusha makiwa,
Makiwa ya baba na mama,
Baba na mama watende,
Wanioza dume kongwe,
Halisafiri halendi,
Kazi kumega matonge (uk. 2).

Wimbo huu haufuati kanuni za arudhi za ushairi wa kimapokeo. Mkusanyiko wa nyimbo hizi za Mnyampala unathibitisha kuwa ushairi wa mwanzo (wimbo) ulikuwa hauzingatii arudhi ya ushairi na nyimbo hizo zilikuwapo kabla ya ujio wa wakoloni. Mbega (1995) anaeleza kuwa kadiri watu walivyojinyakulia mambo mapya ya kigeni ndivyo baadhi ya tamaduni zilivyopotea na kuwa haba ama kumalizika. Hivyo basi, utamaduni wa kigeni au mambo mapya yalisababisha baadhi ya vipengele vya utamaduni kupotea na kuingiza vipengele vya kigeni katika ushairi wa Kiswahili. Vipengele hivyo vilichangia kuleta mabadiliko katika utamaduni wa wenyeji ili kuchukuana na utamaduni huo wa kigeni. Mabadiliko hayo yalisababisha kupoteza mtindo na muundo wa asili wa ushairi wa Kiswahili. Kwa hiyo, arudhi ya ushairi kama vile urari wa vina ilitokana na maingiliano ya tamaduni mbalimbali hususani ujio wa Waarabu na hati ya Kiarabu.

## 5.0 Hitimisho

Kutokana na mjadala huu tumebaini kuwa vipengele mbalimbali vilivyobainishwa katika makala hii vina mchango mkubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mnyampala alikuwa anapenda mabadiliko katika sanaa ya ushairi na hii ndiyo maana alikuwa anajaribu kuibua mitindo na miundo mipya ya utunzi wa ushairi wakati wa uhai wake. Japo Mnyampala alithamini matumizi ya arudhi katika utunzi wa mashairi, alitambua umuhimu wa mabadiliko katika sanaa hii. Bila shaka mtazamo huu wa Mnyampala ndio uliosababisha hata watunzi wengine kufikiria kuleta mabadiliko katika tasnia ya ushairi wa Kiswahili na fasihi kwa ujumla. Hivyo, kutokana na mabadiliko aliyochangia katika ushairi, kazi za ushairi

za Mnyampala ni mfano mzuri wa Nadharia ya Urasmi Mpya katika fasihi ya Kiswahili. Hivyo, mbinu zilizotumiwa na Mnyampala katika utunzi wake zinatumiwa hadi sasa. Ijapokuwa zingine kwa sasa zinatumika katika mtindo mpya kutokana na mabadiliko ya jamii ili kuendana na mabadiliko yaliyopo katika jamii. Kwa ujumla, mchango wake katika ushairi wa Kiswahili hauna kifani.

## Marejeleo

Abedi, A. (1954/1983). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bereau.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books.

Kandoro, S.A. (1972). *Mashairi ya Saadani*. Dar es Salaam: Mwananchi Publishing.

Komba, J.J. (1969). “Mtumishi Wetu Mnyampala.” *Kiswahili.* Juz. 39:1-2.

Kunemah, A. S. (2008). *Misemo na Methali katika Ushairi*. Dar es Salaam: TUKI.

Kyamba, A.N. (2016). “Muundo wa Diwani ya Mnyampala (1965) na Nafasi yake Katika Kuibua Maudhui.” *Kioo cha Lugha.* Juz. 14:96-110.

________ (2018). Mwingilianomatini katika Ushairi wa Mathias Mnyampala. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi.

Mberia, K. (2005). *Radio na Mwezi*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

_______ (2007). *Bara Jingine*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

_______ (2007). *Msimu wa Tisa*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.

Madumulla, J.S. (2011). “Mathias Mnyampala: Jabali Lililosahaulika.” Makala iliyowasiliswa katika Kumbukizi ya Amri Abedi na Mathias Mnyampala (Karimjee, Dar es Salaam). Dodoma: Chuo Kikuu cha Dodoma.

Makaka, E.E. (2012). “Mathias Mnyampala: A Multifaceted Personality.” Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mgute, W. (2012). Mchango wa Mathias Mnyampala katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mmbaga, N.O. (1981). Ngonjera za Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mnyampala, M. (1959). *Fasili Johari ya Mashairi*. Dar es Salaam: East African Swahili Commitee.

_______(1965). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

_______(1965). *Waadhi wa Ushairi*. Dar es Salaam. Oxford University Press.

_______(1966). *Utenzi wa Injili*. Tanzania: Ndanda Mission Press.

_______(1966). *Utenzi wa Zaburi*. Tanzania: Ndanda Mission Press.

_______(1966). *Taaluma ya Kiswahili*. Dar es Salaam: UKUTA.

_______(1968). *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Dar es Salaam: UKUTA.

_______(1970). *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
_______(1971). *Ngonjera za UKUTA Na. 2*. Dar es Salaam. Oxford University Press.
Mnyampala, M. (2011). *Historia ya Hayati Sheikh Amri Abedi Kaluta: 1924-1964*. Dar es Salaam: Ahamadiya Printing Press.
_______(2014). *Maisha ni Kugharamia*. Paris: $DL_2$A-Buluu Publishing.
Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU Dar es Salaam.
Mwangomango, J. (1971). "Ngonjera za Ushairi." *Kiswahili,* Juz. 41(2): 67-71. Dar es Salaam. TUKI.
Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadhari na Mbinu*. Nairobi: JomoKenyatta Foundation.
Nyangwine, N. na Masebo, J. (2002). *Uhakiki Katika Fasihi.* Dar es Salaam: Nyambari Nyangine Publishers.
Nyerere, J.K. (1996a). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Luka*. Ndanda: Benedictine Publications.
_______ (1996b). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Marko*. Ndanda: Benedictine Publications.
_______ (1996c). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Matayo*. Ndanda: Benedictine Publications.
______ (1996d). *Utenzi wa Enjili: Kadri ya Utongo wa Yohana*. Ndanda: Benedictine Publications.
_____ (1996e). *Utenzi wa Matendo ya Mitume*. Ndanda: Benedictine Publications.
Ponera, A. S. (2010). "Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi". Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.
Robert, S. (1959). *Kielelezo cha Fasihi*. Nairobi: Nelson.
_______(1974). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Nairobi: Nelson.
Samwel, M., Seleman, A.J. na Kabiero, A.J. (2013). *Ushairi wa Kiswahili: Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya Mea*. Dar es Salaam: MEVELI Publishers.
Shitemi, L. N. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini*. Eldoret: Moi University Press.
Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
Walibora, K. (2007). *Diwani ya Karne Mpya*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
______ (2004). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers Limited.
Williams, J.C. (1974). "Diwani ya Mnyampala." *Mulika*. Juz. 3:15-23.